TUNAPANA MASHAURI

SIKU NA SAA ZA KUFUNGULA NI:
Siku ya kwanza mpaka siku ya tano tunafungula saa 9 -14

Ukiwa na lazima ya mashauri juu ya kujuwa mambo ya kurudia mu inchi yako unaweza kutupigia simu mu ki-danois na kingereza kwa hii namba: 33 73 50 00

Tunapanaka shauri mu luga ya ki-danois, kibosnia, kiserbia na kikroasia kwa hii namba: 33 73 52 33

Mu luga ya kiharabu, kikurdisti na kisorani, ni hii namba njo yafaa kuita: 33 73 52 28

Kama unataka mashauri mu luga ya kisomalia, tupigie simu kwa hii namba: 33 73 53 11

Kama unataka kupewa mashauri za kipekee kuhusu haki zako kufwatana na kurudia nyumbani inchini mwako unapashwa kujaza hii formulaire ya ma informations zako mbali mbali, yenyi inapatikana ku site internet yetu:

www.atvendehjem.dk

Unaweza pia kutuandikia email kwa hii anuani:
atvendehjem@drc.ngo

DANSK FLYGTNINGE HJÆLP

Swahili

KUHUSU KURUDI NYUMBANI INCHINI MWAKO - MWAKA WA 2021

HABARI KWA AJILI YA WAKIMBIZI, WAGENI NA WALE WENYI KUWA NA URAIA MBILI KUHUSU KURUDIA NYUMBANI MU INCHI YAKO YA KUZALIWA

DANSK FLYGTNINGE HJÆLP

KAMA UNA MAWAZO YA KURUDIA NYUMBANI INCHINI MWAKO

Shirika ya msaada kwa wakimbizi ya Danemark yenyi inapanaka mashauri kwa wanainchi wenyi wanapenda kurudia kwa utashi wao nyumbani mu inchi yao ya kuzaliwa wala inchi ambamo walikuwa na makao zamani. Wakimbizi, wageni na watu wenyi kuwa na uraia mbili (double nationalité =kukuwa na uraia wa Danemark na wa ingine inchi) wako na uwezo ya kupewa msaada ya pesa kama wanarudia nyumbani mu inchi yenyi walizaliwa amo. Kwa kupewa ile msaada wa kipesa inafwatana na wakati gani ulifika hapa Danemark na aina gani ya kartasi ya makao yenyi uko nayo.

Kama unapenda kujuwa mambo yenyi kuhusu kupewa ile msaada kwa kurudi nyumbani mu inchi yako, itabidi ujaze na ututumie formulaire ya habari (formulaire d'informations) yenyi inapatikana kwa hii site internet yetu: www.atvendehjem.dk.

MSAADA YA PESA

Kuanzia mwaka wa 2021 watu wakubwa watakuwa na uwezo ya kupewa pesa elfu:144.900 kr. juu ya kuanza nazo maisha ya mupya mu inchi yako ya kuzaliwa. Watoto wana uwezo ya kupewa pesa elfu: 44.193 kr.

Utapewa zile pesa mu vipindi viwili. Kipindi kya kwannza ni wakati wakusafiri. Mtu mukubwa atapewa elfu: 57.959 kr. na mutoto atapewa elfu: 17.677 kr. Na ingini kipindi mtu mukubwa atapewa elfu: 86.941 kr. na mutoto: 26.516 kr. Izi azo mutazipewa mukisha fanya mwaka moja mu inchi yenu ya kuzaliwa.

ZINGINE NAMNA ZA MISAADA

- Msaada ya safari,
- Usafirishaji wa vitu vyako oa msaada ya kuuza vitu vyako vya kipekee,
- Vyombo vya kufanya navyo kazi fulani na usafirishaji wa vyombo vile,
- Msaada juu ya magonjwa (assurance maladie)/Pesa za matunzo kwa munganga mu muda ya miaka 4,
- Madawa za kutumia mu muda wa mwaka 1,
- Vyombo vya lazia bienyi binaweza kukusaidia,
- Pesa za kulipia batoto masomo mu muda ya miaka 4 kwa watoto wenyi biko mu amri ya miaka 5 mpaka miaka 16,
- Utapewa msaada ya kutafuta makartasi zenyi utasafiri nazo.

DRC DANSK FLYGTNINGE HJÆLP

KAMA ULISHA ENEZA MIAKA 55

Ukiwa na umri wa miaka 55 na unapenda rudia ku nyumba mu inchi yako ya kuzaliwa, unaweza pia kuwa na pewa msaada ya pesa fulani kila mwezi kutoka Danmark.

Ukiwa na umri kati ya miaka 50 na miaka 54, unaweza kufwatana na hali fulani kupewa pia kiasi ya zile pesa.

Msaada ya kupewa kila mwezi ni kati ya elfu: 2.800 kr. na elfu: 3.600 kr. Kwa kupokea ile msaada, inabidi uwe na kartasi za makao ya miaka 5 hapa nchini Danemark.

Ikiwa kuna makubaliano ya nchi mbili kati ya Denmark na nchi yako ya kuzaliwa, unaweza pia kuwa na pewa sehemu ya pesa yako ya pension (pesa ya uzee).

HAKI YA KUBADIRISHA UAMUZI WA KURUDIA MU INCHI YAKO

Wakimbizi wako na haki ya kubadirisha ile uamuzi walikuwa walikamata ya kurudia nyumbani mu inchi yabo ya kuzaliwa na wanaweza rudia hapa Danmark mu muda ya mwaka 1. Kwa wakimbizi ina amanisha kwamba wanaweza rudishiwa kartasi zao za kukaa hapa nchini ya Danemark. Alakini kama wanabadirisha mawazo ya kurudi mu inchi yabo, wataombwa tu warudishe zile pesa za msaada walizo pewa wakati waliomba kurudia ku inchi yabo ya kuzaliwa.

Wageni wao hawana haki ya kurudia Danemark wakati watakuwa walisha rudia mu inchi zao na wakisha pewa msaada ya kurudia kwao. Kwa wageni ile uamuzi ni ya mwisho na ni kusema kwa heri ku haki zenyi wageni walikuwa nazo muda ya makao yao hapa mu inchi ya Danemark.

Uraia mbili (double nationalité) mbele watu wenyi kuwa na uraia mbili waondoke kutoka Danemark, inabidi waache nusu ya uraia wao wa Danemark. Kwa kufanya vile wako na haki ya kubadirisha ile uamuzi ya kupoteza uraia wa Danemark mu miaka 2. Kama munabadirisha mawazo ya kurudia nyumbani mu inchi yenu, itabidi vile vile kurudisha pesa ambazo mulikuwa mulipewa wakati muliomba kurudia inchini mwenu.

KUJUWA ZAIDI

Ikiwa una mpango wa kurudia mu inchi yako ya kuzaliwa, unaweza kujaza na kututumia formulaire ya information yenyi inapatikana ku site internet yetu. Wakati tutafaya mukutano wa kipekee, tutakuelezea mambo yenyi kuhusu haki zako, juu upate ginsi ya kukamata uamuzi wako. Kama unaitaji mtafsiri, tutaweza kukuletea aye. Kazi yetu sisi nikukupa information zenyi utatumikisha kwa kumata uamuzi wako.